**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MJI KOROGWE**

**SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KOROGWE**
S.L.P 155 Korogwe-Tanga, Barua pepe:acakorogwesec2021@gmail.com, Simu/Contcts:
Mkuu wa Shule-0769036380, Makamu Mkuu wa Shule-0745702226, 0710542504

---

**Kumb.Na. KGSS/A/24/04/2024** **Tarehe:24/04/2024**

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi:……………………………..
…………………………………………………………...
S.L.P……………………………………………………..
……………………………………………………………

## YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA KOROGWE MWAKA 2024/2025

**1.0.** Nafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na **kidato cha tano** Tahasusi ya ………….. katika shule hii mwaka **2024/2025**. Shule ya sekondari ya Wasichana Korogwe ipo umbali wa Kilometa moja kutoka kituo cha mabasi cha mji wa Korogwe. Usafiri wa Bajaji/pikipiki unapatikana katika kituo cha mabasi cha Mji wa Korogwe. Nauli ni shilingi elfu moja.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe ***……/……/2024*** Unatakiwa kuripoti kuanzia tarehe ***……/......2024.*** na mwisho wa kuripoti ni tarehe ***…../…../2024.***

## 2.0.Mambo muhimu ya kuzingatia;-

### 2.1.Sare za Shule

(a) Sare ya shule hii ni;-.

(i) Sketi mbili mshono wa rinda boksi kitambaa kizito(Kitambaa cha suti) ifike kwenye kiwiko cha mguu - Rangi ya 'Orange '.(**Mwanafunzi atakaye kuja na sketi isiyokidhi vigezo haitapokelewa)**
(ii). Nguo ya kazi (Shamba dress) moja(1) rangi ya bluu bahari (Mshono wa kijola wenye Mifuko miwili ya kubandika).
(iii). Sweta rangi ya kijivu (Grey).
(iv) T-Shirt ya rangi ya kijivu(Grey) yenye nembo ya shule.(Inapatikana shuleni).
(v). Mashati mawili meupe (Tetron) mikono mifupi.
(vi). Nusu kanzu (Rangi nyeupe) inayofika mapajani.
(vii) Hijabu rangi nyeupe (tetron) kwa ajili ya darasani.
(viii) Hijabu rangi nyeusi (tetron) kwa ajili ya nje ya darasa.
(ix) Sare ya viatu vya darasami ni viatu vyeupe au raba nyeupe ambavyo havina kisigino (Jozi mbili) aje navyo.
(xi) Soksi jozi mbili au zaidi nyeupe.
(xii). Sketi mbili za blue iliyokolea (dark blue) za kuvaliwa nje ya darasa mshono wake ni rinda boksi na ifike kwenye kiwiko cha mguu (**Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo ya nyumbani**)

NB : Iwapo mzazi/Mlezi utashindwa kushona sare ya mwanafunzi kwa sababu yoyote ile, basi mwanafunzi anaweza kushona sare hizo kwa fundi wa nguo anayepatikana shuleni kwa gharama zifuatazo :-

i. Sketi mbili za rangi ya orange – Shs 44,000
ii. Nguo ya kazi(Shamba dress) moja – Shs 22,000
iii. Mashati mawili meupe – Shs 18,000
iv. Sweta la Shule rangi ya kijivu – Shs 15,000
v. T-Shirt ya rangi ya kijivu(Grey) yenye nembo ya shule – Shs 10,000

(b) Sare ya michezo kwa shule hii ni kama ifuatavyo;
(i). T-sheti nyeupe isiyo na picha, mchoro wala maandishi.
(ii). Bukta rangi yoyote inayofika kwenye magoti.
(iii). Sketi fupi ya marinda rangi ya zambarau (purple) ya kuvaa juu ya bukta (Inayofika kwenye magoti).
(iv). Raba nyeusi.

**2.2 Mahitaji Mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni;-**
(i) Ndoo mbili(lita 10) zenye mfuniko, sahani, kijiko na kikombe.
(ii) Koti la mvua au mwamvuli.
(iii) Shuka mbili au zaidi za rangi ya pink na blanketi moja.
(iv) Taulo, malapa, mswaki, kanga/vitenge viwili,Mto (Foronya ya mto ifanane na rangi ya shuka), nguo ya kulalia nyepesi na mahitaji mengine muhimu ya mtoto wa kike.(Kikoi au shuka la kimasai haviruhusiwi)
(v) Chandarua kimoja cha pembe nne.
(vi) Tracksuti ya rangi ya blue iliyokolea (dark blue) kwa ajili ya kujikinga na mbu wakati wa kujisomea usiku.
(vii) Madaftali makubwa yasiyopungua 14, kalamu za kutosha na mathematical set moja.
(viii) Vitabu vya dini na mahitaji mengine ya dhehebu la mwanafunzi.
(ix) **Ream ya Karatasi (A4) mbili (2)** kwa mwaka. (Kampuni ya **A(1)ONE** au nyingine isiwe kampuni ya MONDI)
(x) **Kwa wanaosoma somo la Chemistry waje na (Digital stop watch** pamoja na **Scientific Calculator).**
**(xi) Kwa wanaosoma somo la Biology mwanafunzi aje na Dissecting kit.**
**(xii) Aje na kadi ya Bima ya Afya. Kama hana bima ya afya awe na fedha binafsi ya dharura.**

**2.3 Michango mbalimbali;**

(a)

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

(b) **TZS 10000/= kwa mwaka kwa ajili ya kukodisha godoro.**

**N.B**. ***Fedha hiyo yote Jumla Tshs 90,000/- (a. na b.) ilipwe kwenye Akaunti ya shule namba 41501100013 NMB kwenye tawi lolote na mwanafunzi aje na risiti ya malipo ya benki ikiwa imeandikwa jina sahihi la mwanafunzi.***

**2.4 Vifaa vya Usafi**

- **a)** Tahasusi ya **CBG** walete **Jembe lenye mpini, Ufagio wa chelewa**, **hard broom** na **Toilet brush.**
- **b)** Tahasusi ya **PCB** walete **Jembe lenye mpini, Ufagio wa chelewa**, **hard broom** na **Toilet brush.**
- **c)** Tahasusi ya **PCM** walete **Jembe lenye mpini, Ufagio wa chelewa**, na **Mopper na Ndoo yake**
- **d)** Tahasusi ya **HGK** walete **Jembe lenye mpini, Ufagio wa chelewa**, na **Toilet brush na soft broom**
- **e)** Tahasusi ya **KLF** walete **Jembe lenye mpini,Ufagio wa chelewa**, **Toilet brush** na **Squeezer**
- **f)** Tahasusi ya **HKL** walete **Jembe lenye mpini, Ufagio wa chelewa**, **soft broom** na **Toilet brush.**
- **g)** Tahasusi ya **HGL** walete **Jembe lenye mpini, Ufagio wa chelewa**, **Soft broom**, na **Sqeezer**
- **h)** Tahasusi ya **HLF** walete **Jembe lenye mpini, Ufagio wa chelewa**, na **Reki**
- **i)** Tahasusi ya **HGF** walete **Jembe lenye mpini, Ufagio wa chelewa**, **hard broom**, na **Sqeezer**

## 3.0 Sheria na Kanuni Muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b). Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
(c). Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation).
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(i) Mwanafunzi atakapofika shuleni awe amekata nywele robo nchi na zisiwe zimewekwa dawa. Shuleni hakuna kusuka nywele.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).
- ❖ **Mwanafunzi haruhusiwi kuja na pambo la aina yoyote.(Mkufu,heleni, pete n.k)**

**3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha Mwanafunzi kufukuzwa shule**

1. Wizi

2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
3. Kutoa lugha Chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
4. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
5. Uasherati, Mahusiano ya jinsi moja.
6. Ubakaji.
7. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, uvutaji wa Sigara, Cocaine, milungi, kubeli n. k.
8. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
9. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
10..Kushiriki matendo ya uhalifu na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
11. Kudharau bendera ya Taifa
12. Kuoa au kuolewa
13. Kupata mimba, kutoa mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
14. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
15. Kukataa adhabu kwa makusudi.
16. Mwanafunzi kumiliki simu ya mkononi, redio na pasi ya umeme au kifaa chochote kinachotumia umeme.
17. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

**4.0 Viambatisho na Fomu muhimu**

(a) Fomu ya uchunguzi wa afya (Medical examination form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(c) Fomu ya Mzazi/Mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa michango na maelekezo mengine yatolewayo na shule.

**5.0** Tafadhali soma kwa makini maelezo/Maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**A M MAUKA**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA
KOROGWE

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule - 0769-036380**
- **Makamu Mkuu wa Shule- 0745-702226**
- **Mwandamizi Taaluma – 0710-542504**
- **Mwandamizi Malezi - 0688-102786**

# PRESIDENT'S OFFICE
# LOCAL GOVERNMENT AND REGIONAL ADMINSTRATION
# KOROGWE TOWN COUNCIL
# REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**KOROGWE GIRLS**
**SECONDARY SCHOOL**
**P. O. BOX 155,**
**KOROGWE.**

**DATE………………………**

**MEDICAL OFFICER,………………….. GOVN. HOSPITAL,**
**………………………………………………………………..**

**NAME OF STUDENT……………………………………………………………………………..**
Please examine the above named girl to ascertain her fitness for further studies.

**………………………**
**HEADMISTRESS**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA
KOROGWE

## MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by the medical officer)
I have examined the above named with regard to:
Skin…………………………………………………………………………………………….
Eyes…………………………………………………………………………………………….
Ears……………………………………………………………………………………………..
Chest…………………………………………………………………………………………….
Spleen…………………………………………………………………………………………...
Abdomen………………………………………………………………………………………..
Urine…………………………………………………………………………………………….
Stool…………………………………………………………………………………………….
Hemoglobin……………………………………………………………………………….....

**And I considered:**

1. She is good health, free from infection diseases, worms, bilharzias and fit to go to school.
2. She is now fit to return to school having treatment for………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………………
   NAME AND SIGNATURE OF MEDICAL OFFICER DATE

**And I considered:**

3. She is now fit to return to school having checked for……………………………………………
   ………………………………………………………………………………………………
   ……………………………… ……………….……… ………………………
   NAME AND SIGNATURE OF MEDICAL OFFICER DATE

# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA MJI KOROGWE

KOROGWE SEKONDARI
S. L. P. 155,
**KOROGWE.**

## (C): FOMU YA KUKUBALI NAFASI ALIYOPEWA

**SEHEMU A:** Habari za Mwanafunzi.

1. Jina kamili…………………………………………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa…………………………………………………………………..
3. Wilaya alipozaliwa………………………………….. Kijiji …………………………
4. Kukubali nafasi (Ijazwe na mwanafunzi)

Mimi …………………………………………… nimeona maagizo yote ya kujiunga na shule ya Sekondari ya Wasichana Korogwe na ninakubali kutimiza masharti yote ya shule ikiwa ni pamoja na uletaji wa vifaa vinavyohitajika na kutii sheria zote za shule. Nitakapokuwa shuleni Korogwe nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kuzingatia yote ambayo wanafunzi wanatakiwa kutimiza katika suala zima la kupata Elimu ya kujitegemea.

**Sahihi ya Mwanafunzi…………………………　　　　Tarehe………………………..**

**SEHEMU B**: Habari za Mzazi/Mlezi (Ijazwe na Mzazi/Mlezi)

1. Jina kamili………………………………………………………………………………
2. Yeye ni Mzazi/Mlezi…………………………………………………………………
3. Kazi yake ……………………………………………………………………………..
4. Anwani ya Mzazi/Mlezi

………………………………………………………………………
………………………………………………………………………
……………………………………………………………………..

5. Namba tatu za simu ikiwemo ya Mzazi/Mlezi na ndugu wa karibu wa Mwanafunzi
   (a)………………………………………………………………………………………
   (b)……………………………………………………………………………………….
   (c)……………………………………………………………………………………….

### UTHIBITISHO

Mimi Mzazi/Mlezi wa ………………………………………………………. nimehakikisha kwamba maagizo yote yemeeleweka na mtoto wangu amejaza kikamilifu sehemu A.

**Sahihi ya Mzazi/Mlezi………………………..　　　　Tarehe…………………**